

# tambua chaguo yako, fahamishwa

Swahili | Kiswahili

## Kulazimishwa kuzala ni nini?

Kulazimishwa kuzala na unyanyasaji ni tabia inayokusudia kuweka mamlaka na uzibiti (controle) kwa kuingilia uhuru wa uzazi wa mtu mwenye kuwa na mimba, kuzibiti (ku controler) na / au kuingilia maamuzi na upatikanaji wa chaguo kuhusu afya ya uzazi na chaguo ya uzazi.

Kulazimishwa kuzala na unyanyasaji unaweza kujitokeza kupitia:

### Kukazwa kubeba mimba

Iyi inaweza kuwa kama:

"Kama uko na mtoto wangu, nitajua kama unanipenda kweli kweli"

"Kama tuko na mtoto pamoja, nakupa ahadi kwamba bitu bitakuwa muzuri"

"Tunaowana, kwa nini hauko nabeba mimba?"

"Kama uko na mtoto, ataleta furaha katika familia yangu"

### Kuzibiti uamuzi wako wa kuendelea au kutosha mimba

Iyi inaweza kuwa kama:

"Kama unanipenda, utanizalia mtoto"

"Nataka mtoto mwanaume/ mwanamuke, tutaendelea kuzala mpaka siku tutapata mtoto mwanaume/mwanamuke"

"Kama unazala uyu mtoto, utaleta haya kwangu na kwa familia yangu"

### Kuficha, kutosha au kutupa dawa za kupanga uzazi au kuzuwia kubeba mimba

Kutosha dawa ya kupanga buzazi kutoka katika mwili wako.

Kuacha kulipia au kusimamisha malipo ya kupanga uzazi.

Kutobola matundu katika condom (capotte katika kifaransa) au kutosha condom wakati wakufanya mapenzi.

"Sipendi utumiye kinini ao aina yoyote ya kupanga uzazi"

"Ukitumia aina yoyote ya kupanga uzazi nitakuacha"

"Sijisikiyake muzuri nikitumikisha condoms, sitazitumikisha"

"Tuliisha owana, hatuna lazima ya kuvala condom ao kupanga buzazi"



Kulazimishwa kuzala ni aina ya unyanyasi, ili upate msaada unaweza kusumulia na Children by Choice (Watoto kwa Kutaka) ku 1800 177 725  
[www.childrenbychoice.org.au](http://www.childrenbychoice.org.au)

CHILDREN  
BY CHOICE  
ASSOCIATION INCORPORATED

